

Maoni yangu kuhusu sahaba

Je sahaba ni nani?

Kwa mujibu wa taarifa ya Imam Ibn Hajar al-Asqalani, iliyomo uk. 10 wa Juzuuy ya Kwanza ya kitabu chake kiitwacho al-Isaba, 'sahaba ni yule aliyemkuta Mtume (s.a.w.w), sahaba ni yule aliyemuona Mtume akawa amemwamini, na akafa katika Uislamu.

'Hivyo, kwa waliomkuta (Mtume s.a.w.w.), aingia yule aliyekaa naye muda mrefu au mfupi; (aingia) na yule aliyepokea kwake au hakupokea; (aingia) na yule aliyepigana jihadi pamoja naye au hakupigana; na yule aliywona kwa macho japo iwe hakukaa naye, na (hata) yule ambaye hakumwona kwa kizuizi kama (cha) upofu.'

Ibn Hajar katika uk. 5 wa Juzuuy ya Saba ya Fathul Bari, amesema kwamba imepokewa kwa Ali b. al-Madini kuwa amesema: 'Yeyote aliyefuatana na Mtume (s.a.w.w) au aliywona japo ni kwa saa moja mchana, ni miiongoni mwa sahaba wa Mtume s.a.w.w.'

Na Imam Nawawi naye, katika uk. 14 wa Juzuuy ya Kwanza ya Tahdhibul Asmaa Wal Lugh-ghaat, amesema: 'Kuhusu sahaba kuna madhehebu mbili: lililo muhimu kati yayo — nayo ni madhehebu ya Bukhari na wanazuoni wengine wote wa Hadith, na jamaa katika wanazuoni wa fiqhi na wasiokuwa wao — ni kwamba kila Mwislamu aliywona Mtume s.a.w.w. japo ni kwa saa moja, na hata kama hakukaa naye na kuingiliana naye, (ni sahaba).'

Tunaposoma uk. 4 wa Juzuuy ya Saba ya Fathul Bari na uk. 12 wa Juzuuy ya Kwanza ya al-Isaba, tunamwona Imam Ibn Hajar al-Asqalani akisema: '...Lau mtu aliritadi, halafu akarejea katika Uislamu, lakini akawa hakumwona (Mtume s.a.w.w.) mara ya pili baada ya kurejea kwake (Uislamuni); lililo sahihi ni kwamba (mtu) huyo huhesabiwa ni sahaba kwa vile ambavyo wanazuoni wa Hadith wamemuhesabu hivyo Ash'ath b. Qays na mfano wake.

KISUNNI sahaba ni;

- (i) yeyote yule aliywona Bwana Mtume s.a.w.w. na akafa hali yu Mwislamu;
- (ii) wala si lazima awe amekaa naye sana, bali hata kama amemwona kwa saa moja tu inatosha;

(iii) na wala si lazima awe ni mtu mzima, bali hata kama alimwona utotoni au uchangani, na hata kama alikuwa bado yu utotoni au uchangani wakati Bwana Mtume s.a.w.w. alipofariki dunia; na

(iv) hata kama mtu huyo aliritadi, kisha akarejea Uislamuni, lakini asiwahi kumwona tena Bwana Mtume s.a.w.w. baada ya kurejea kwake huko!

Je sahaba wote ni waadilifu? Na je sahaba hawafanyi makossa? Na je haifai sisi kuzungumza yalewaliyoyafanya?

Imani yangu ni kuwa baadhi tu ya sahaba ndio waadilifu, na baadhi nyingine si waadilifu. Naamini kuwa wako masahaba wengi waliokuwa watu wazuri sana, na naamini pia wako baadhi yao waliokengeuka na kumuasi Mola wao kama binadamu wa kawaida. Kwa mfanoo;

(i) Qudaama b. Madh'un: Huyu ni mionganini mwa Waislamu wa mwanzo mwanzo. Alihama hijra mbili, akawahi hata kupigana katika Vita vya Badr. Lakini pamoja na yote hayo aliwahi kushikwa amelewa, zama za Ukhilifa wa Umar b. al-Khattab, akapigwa haddi! Jee, sahaba huyu bado ni mwadilifu? (Taz. al-Isaba, Juzu ya Tatuu, uk. 219-221; na al-Isti'ab, iliyo chini ya al-Isaba, Juzu ya Tatuu, uk. 247-251)

(ii) Abdulrahman (al-Awsat) b. Umar b. al-Khattab: Huyu, kama jina lake lioniyeshavyo, alikuwa ni mtoto wa Khalifa wa Pili, na alikuwa ni sahaba vile vile. Yeye naye alikamatwa amelewa, na babake akampiga haddi! Hata inasemekana kwamba alikufa kwa kipigo hicho. (Taz. uk. 405-406 wa Juzu ya Pili ya al-Isaba; na uk. 395-396 wa Juzu ya Pili ya al-Isti'ab, iliyo chini ya al-Isaba) Jee, na huyo naye atakuwa ni mwadilifu?

(iii) Abu Mihjan: Huyu ni sahaba mwingine aliyejkuwa akinywa pombe sana na kuzini; hata imeeelezwa kwamba Khalifa Umar b. al-Khattab aliwahi kumpiga viboko mara saba au nane kwa hilo! Akawahi hata kumfunga! (Taz. al-Isaba, Juzu ya Nne, uk. 173-175; na uk. 181-187 wa Juzu ya Nne ya al-Isti'ab iliyo chini ya hiyo al-Isaba.) Jee, sahaba kama huyo vipi huendelea kuwa mwadilifu?

(iv) Nu'aiman b. Amr. Huyu ni sahaba ambaye amepigana jihadi vita vyote. Lakini pamoja na hivyo, alikuwa mlevi! Mara nne Mtume Muhammad' s.a.w.w.

alimkamata sahaba huyo amelewa! Kati ya hizo, mara tatu alimpiga haddi! Mara ya nne, ndipo Umar b. al-Khattab alipotaka akatwe kichwa chake, lakini Bwana Mtume s.a.w.w. hakumkubalia. (Taz. chini ya jina la Marwan b. Qais al-Aslami katika uk. 384 wa Juzuuy ya Tatu ya al-Isaba; na pia juzuuy hiyo hiyo, uk. 540-541, chini ya jina la huyo Nu'aiman. Vile vile taz. Usudul Ghaba, Juzuuy ya Nne, uk. 199 - 200, na Juzuuy ya Tano, uk. 36 - 37.)

(v) Samura b. Jundub: Huyu ni mmoja ya wale watatu walio ambiwa na Bwana Mtume s.a.w.w. kwamba, wa mwisho wao kufa, ataingia Motoni. Yeye alikiuza pombel (Taz. chini ya Hadith Na. 61 katika uk. 82-84 wa Mujallada wa Kwanza wa Silsilatul Ahadithidh Dhaifa Wal Mawdu'a ya Muhammad Nasiruddin al-Albani.)

(vi) al-Walid b. Uqba: Huyu ndiye yule ambaye Mwenyezi Mungu amemwita fasiq katika Sura 32:18 na Sura 49:6. Isitoshe; na ndiye yeye, pale alipokuwa Gavana wa mji wa Kufa zama za Ukhilifa wa Uthman bin Affan, aliyeswalisha watu swala ya asubudhi rakaa nne, na huku amelewa! Kisha akatapika kibulani, akatoa salamu na kuwauliza walioswali naye: Jee, niwaongezee? Kwa hivyo akapigwa haddi na kuondolewa kwenye Ugavana!

Ibn Abdilbar amesema amesema kwamba hakuna hitilafu baina ya wanazuoni kuwa aya hiyo iliteremshwa kwa ajili yake sahaba al-Walid bin Uqba, kama ilivyo tajwa katika uk. 601 wa Juzuuy ya Tatu ya al-Isaba.

Je Mtume kasemaje kuhusu Masahaba?

Turejee Sahih Bukhari na Sahih Muslim:

(i) Imepokewa kwa Anas kwamba Mtume s.a.w.w. amesema: Watu mionganii mwa sahaba zangu watanijia kwenye Hodhi[7]. Nitakapowaona, na watakapokuwa waletwa kwangu, watazuiwa ili wasinifikie. Hapo nitasema: Sahaba zangu, sahaba zangu! Nami nitaambiwa: Wewe hujui walizua nini baada yako.

Hadith hiyo utaiona katika Sahih Muslim, 'Kitabul Fadhaail', Mlango wa 'Hawdhu Nabiyyina (s.a.w.w) Waswifaatuhu.' Kwa Kiingereza ni Hadith Na. 5706 kwenye ukurasa 1239 wa Juzu ya Nne.

Hali kadhalika, Hadith yenye maneno karibu kama hayo yaweza kuonekana katika Sahih Bukhari, 'Kitaabur Riqaaq', Mlango wa 'al-Hawdh'. Na kwa Kiingereza, ni hadith namba Na. 584 kwenye uk. 381 wa Juzu ya Nane.

Hitimisho

Mimi naamini kuwa kuna baadhi ya sahaba ambao, walismama katika mwendo wa sawa na wengine walikengeuka baada ya Bwana Mtume (s.a.w.w. kufariki dunia). Baadhi yao walizua mambo kinyume cha dini yake; ndiyo sababu wasiruhusiwe kumfikia hata baada ya yeye mwenyewe kukumbusha kwamba hao walikuwa sahaba zake!

Ma hiyo ni nature ya binaadamu wote. Wengine husimama mstari wa sawa na wengine hupotoka. Kwani wao hawakuwa Malaika!

Je tuyazungumze ya masahaba au tusiyazungumze? Sisemi tuwatukane!

Kwangu ni muhimu sana kuyasimulia yaliyofanywa na masahaba bila ya kupendelea na kutia chumvi!

Kwa mfano, inajulikana kwamba mionganini mwa sahaba wako waliomsingizia bibi Aisha, mke wa Bwana Mtume (s.a.w.w) mambo machafu!

Wako waliotoka msikitini, wakamwacha Mtume (s.a.w.w) anahutubu juu ya mimbari siku ya Ijumaa, na wao wakakimbilia biashara

Mwisho

Mwenyezi Mungu anasema;

تِلْكَ أُمَّةٌ قَدْ خَلَتْ مَعَهَا مَا كَسَبَتْ وَلَكُمْ مَا كَسَبْتُمْ وَلَا تُسْأَلُونَ عَمَّا كَانُوا يَعْمَلُونَ

'Hao ni watu walio kwisha pita. Watapata waliyo yachuma, nanyi mtapata mtakayo yachuma; wala hamtaulizwa nyinyi waliyo kuwa wakiyafanya wao'

Naamini kuwa wengi wa masahaba walikuwa ni watu wema sana na Mola amewardhia na atawalipa mema kwa kazi kubwa waliyoifanya ya kuuhami Usilamu na kumfuata Mtume Muhammad (s.a.w.w) na wakajitolea mali zao na maisha yao.

Msimamo wangu ni wa kati na kati, na maana yake ni kuwa, si vibaya nionavyo kuyazungumza mambo yaliyopita kwa na kati ya masahaba. Naamini pia kuwa ni vibaya kuwatukana na kuwalaani bila ya kosa lolote ambalo hawakulifanya. Naamini pia ni vizuri kuzungumza yaliyopita kati yao kwa ajili ya kupata ibra na mazingatio katika maisha yao. Siamini kuwa kukaa kimya ndio tiba. Kama kuna sahaba alifanya jambo jema ni vizuri kulisimulia, na kama kuna aliyefanya bayaa pia ni vizuri kulijua. Kama kuna aliyeritadi ni vizuri kujua huyo alikuwa nani na kwa nini? Mwendo huu utatusaidia kurekebisha mambo katika masiha yetu, kwani mara nyingine isi hujifunza kutokana na makossa ya watu wengine. Kama inavyosemwa ‘we learn through mistakes!

Mola awalipe mema maswahaba wema na akipenda kuwasamehe waliomkosea basi Yeye Allah ni Rauufun Rahiim.

Si kazi yangu mimi kumuingiza yejote kati yao peopni au motoni!

Ayub Rashid